KODI JUU YA VYAKULA IMEPIGWA MARUFUKU.

Kutoza ushuru juu ya vyakula mbali mbali kunako soko kuu ya Kadutu kumepigwa marufuku na mnyampara wa Bukavu, mwananchi Ndala wa Ndala.

Azimio hilo lilichukuliwa na mnyampara wa mji wa Bukavu kutokana na uhaba (rareté) wa vyakula bila kusahau harakati za wale jamaa wanayo tabia mbaya ya kuangamiza wakaaji wakiwafyonza mali zao.

Hatua hiyo yaambatana na ile ya prezidenti wa Chama jimboni aliye pia liwali wa jimbo la Kivu, inayopinga usafirishaji wa vyakula katika nchi za kigeni na kusulubisha hivi wakaaji pamoja na wafanyabyashara.

Baada ya kutangazwa kwa hatua hiyo kunako soko kuu ya hapa Bukavu, wachuuzi pamoja na wanunuzi walimpigia mnyampara wa mji wa Bukavu aksanti na kumtolea kelele ya shangwe kufuatana na furaha iliyowajaa moyoni mwao. Wanunuzi pamoja na wachuuzi waweza sasa kuishi kwa amani na kuuza (vendre) vyote wanavyo kwa bei rahisi.

kuuza (vendre) vyote wanavyo kwa bei rahisi.

Kwa kuimarisha maisha ya wanunuzi pamoja na ile ya wachuuzi sokoni, mwananchi Ndala wa Ndala aliwafukuza kwa upanga mkali wa mapinduzi watumishi wa serikali wanohusika na mazingara (environnement), wale wa chumba cha usafi (hygiène), wale wa mambo ya uchumi (économie). Bila kusahau watumishi wanaohusika na kuchungua byashara vinavyovuka mipaka ya nchi yetu (OFIDA).

Kodi iliyokuwa ikilipwa juu ya magari ya uchukuzi wa vyakula (hasa mihogo) imepigwa pia marufuku. Ni wale wachuuzi wa reja reja tu ndio watakuwa wakilipa kodi kila mwaka (patente). Na ni wale watumishi waliopewa kazi hiyo na mnyampara wa Bukavu ndiwo watakuwa na kazi ya kukongowa feza hizo. Ni pamoja na wananchi Bendera na Bashizi ambao watasaidiwa kazini mwao na viongozi wa Chama sokoni. Hakuna mwengine atakayejitatanua kuwa ana madaraka ya kuomba feza sokoni. Mwenyi atakayenaswa katika kosa hilo yafaa apelekwe mbele ya waamzi.

Twazani kuwa magumu ya kupata mihogo na vifaa vingine katika soko kuu la Kadutu itaweza kupunguka na kuwa bei ya unga wa mihogo inayorukaruka kila mara itaweza kupunguka. Tunatumaini pia kuwa watumishi wa kazi za serikali wanaohusika na kuheshimisha bei ya bizaa watatupilia mbali pupa kali yao ya feza ili wakaaji wapate kupumua na kufurahi na uongozi mwema wa nchi yetu.

Bisimwa L-B Tserou
na Kaboyi Habimana

JUA
Gazeti la Kivu

MUUAJI CHIFENDE BENGEHYA KASULUBIWA !

Munguana husema: siku za mwizi ni arubaini na damu ya binadamu haimwangike bure.

Kulingana na masemi hayo, mnamo tarehe 4 februari 1985, fundi-mwizi Chifende Bengehya alitiwa kwenye ngoti mbele ya umati mwingi wa watu pande za saa tano kunako jela kuu la jimbo mjini Bukavu.

Kutungikiwa kwa mwizi Chifende aliyekuwa na umri wa miaka 6 ya kifungo kulifanyika kisha Baba wa taifa kukataa maombi yake ya kuomba huruma.

Hatua hiyo ilichukuliwa na serikali ili kutoa fundisho kwa wananchi wote wanayo pupa ya kuwina mbio wasijue tabu wengine walipata kwa kufikilia kupata mali zao.

CHIFENDE KAFIA NINI ?

Usiku wa tarehe 18 na 19 Desemba 1979, kikundi cha wizi kikashambulia makao ya wananchi Zigize Mwitigerange na kumshika mateka. Ukomo wa mshambulio hayo haukuwa ungine bali ni ule tu wa kunyanganya kiasi cha feza za kulipa watumishi wa shamba la Lushasha aliyokuwa akiongoza marehemu huyo.

Bila huruma, marehemu Zigize alipigwa risasi tatu na mnyanganyi Chifende akajiruhusu bila wasi wasi wote kumtoa pumzi lote akimkunguta shoka kwenye shingo.



Hapa pichani mwaona mlingoti (potence) ambako hutungikwa watenda maovu kama vile wauaji. Mlingoti huu pichani ni ule upatikanao katika jela moja nchini Ujerumani Mangharibi.

Baada ya kufungwa, mnamo tarehe 6 marsi (mwezi wa tatu) 1981, Korti kuu la mji wa Uvira likahukumu muuaji Chifende kifo na hukumu hilo likakamilishwa na Korti la mwisho (Cour d'Appel) la jimbo la Kivu, mjini Bukavu kulingana na hatua yake ya tarehe 1 aprili (mwezi ya nne) 1982.

Ni hivi wakuu wa serikali jimboni wakahukumu muuaji Chifende atiwe kwenye mlingoti (potence) alipe makosa yake mnamo tarehe 4 februari 1985 kunako Jela la Kivu la mji wa Bukavu.

Iligeuzwa na
BISIMWA L-B. Tserou.

Bagira

AMULI SEBUHOME AMEPIGWA BAKORA YA MAPINDUZI.

Habari zinazoaminika kutoka ofisi ya mkuu wa jimbo zinaeleza kuwa mwananchi Amuli Sebuhome, makamu wa kiongozi wa mtaa wa Bagira (Commissaire de zone assistant) amejionea kweli cha mtema kuni.

Inasemekana kuwa prezidenti wa chama chetu cha Mapinduzi jimboni aliye pia liwali wa jimbo la Kivu, mwananchi Mwando Nsimba alishikwa na hasira na akampiga Amuli Sebuhome bakora ya kimapinduzi kwa kumuachisha kazi mpaka akabaki kinwa wazi akishindwa hata kunena lolote na kujipiga kifuani ginsi anavyozoea kufanya.

Alipewa malipizi hayo kutokana na kosa kubwa alilotenda wakati alipojiruhusu kuachilia huru majambazi pamoja na wayanguyangu walionaswa mnamo usiku wa siku ya posho tarehe 9 kuamkia siku ya Mungu tarehe 10 februari 1985. Bagira anakoishi, watu husema kuwa yule anayezoea kujitatanua akisema eti yupo mwenyi maarifa (intellectuel) na mwerevu kushinda wote (clair) ana mazoezi ya kutenda mambo kama yale kusudi vichele vilie mfukoni mwake.

Wale wanaomfahamu vema mwananchi Amuli Sebuhome waeleza kuwa ni mla pipa na mkorofi wa ajabu ambaye hawezi kurudi nyuma mbele ya feza haizuru ngapi. Wengine hunongone huko Bagira ambako amegeuka mwami wa Batwa eti makosa yake ni mengi, na mengine ya haya.

Heko kwako liwali Mwando kwa kuchukua hatua kali kama hiyo. Lakini uwe tu "macho wazi" kwani wafuasi wa Amuli Sebuhome ni wengi na waendelea kujificha. Yafaa kuwagundua na kuwaonyesha nao kile wangwana wanachozoea kuita "cha mtema kuni". Wanafiki (hypocrites) nao wapigwe marufuku na wabaki wenyi kujuta kama mtoto aliyepasua kibuyu cha maji. Mfano kwao ule wa Amuli Sebuhome!

KABOYI HABIMANA

KUTAFUTA NDUGU

Mwananchi Mukambilwa Basilwango Uratho, anamtafuta mkubwa wake anayejulikana kwa jina la Mukambilwa Mutembo Kasonga. Mkubwa wake huyo alijielekeza mnamo mwaka wa 1973 huko Lubumbashi (Shaba) kusudi ya kuendelesha masomo yake. Tangu mwaka 1976 mpaka sasa hafahamu nafasi apatikanapo.

Kwa hiyo, mwananchi Mukambilwa Basilwango Uratho anamuomba yeyote anayemfahamu ndugu yake huyo amjulishe habari zake akitumia anuani ya gazeti JUA ambayo ni kibweta cha posta 1613 Bukavu.